# UNYANYASAJI WA WATOTO

Tazama, wana ndio urithi wa BWANA, uzao wa tumbo ni thawabu. Kama mishale mikononi mwa shujaa, ndivyo walivyo wana wa ujanani. Heri mtu yule aliyelijaza podo lake hivyo. Naam, hawataogopa wanaposema na adui langoni, Zaburi 127:3-5

Moja ya nyakati za furaha maishani mwangu ni kuongea na watoto wangu. Tangu vizazi na vizazi imesemwa kuwa watoto hudhihirisha upendo. Kwa kadri tunavyoongea na watoto wetu, swali linalotakiwa kuulizwa ni kwamba tunaongea nao katika wakati muafaka? Wengine hutumia muda wao kuongea na watoto wao, lakini kwa kuwanyanyasa na kwa hiyo watoto wengine wanafanyiwa unyanyasaji wa kimwili, kingono na kiroho.

Unyanyasaji wa kimwili

Unyanyasaji wa kimwili kwa watoto ni jambo lililozoeleka. Jamii za kale na tamaduni nyingi katika ulimwengu huu bado hufubia macho unyanyasaji wa kimwili kwa watoto. Wanajisikia na kuamini kuwa ni sahihi. Na kwa kweli, jambo hili liliachiliwa litokee hata Marekani hadi kizazi kimoja au viwili vilivyopita wakati serikali ilipoanza kutunga sheria dhidi ya unyanyasaji wa watoto. Unyanyasaji wa kimwili hufanywa kwa namna mbalimbali. Kuwa katika mazingira hatarishi nyumbani, kupika chakula ambacho hakifai, kuvaa vivazi visivyo vya heshima, kuwashurutisha watoto kuvuta moshi wa sigara, kuwazidishia kazi watoto, kutumia fedha kwenye pombe, sigara, kamali na dhambi zingine wakati watoto wanabaki bila mahitaji muhimu, yote haya na mengineyo ni unyanyasaji wa kimwili. Halafu yapo matukio mabaya zaidi ya ukatili wa kimwili.

Katika matukio mengi, unyanyasaji ni matokeo ya jambo lililoendekezwa. Hakuna ubaya, kwa kweli tunatakiwa kuwahimiza watoto wetu kwa kuwafundisha kupata vipato vyao kwa jasho la kope za macho yao, Mwanzo 3:19. Lakini hawakuumbwa ili wawe watumwa. Tunaagizwa kuwaadhibu watoto, Mithali 23:13, lakini hili linatakiwa lisifanyike huku ukiwa na hasira. Sisi kama wazazi lazima tuchukuliane na watoto wetu, na kukumbuka sheria za dhahabu, kuwatendea watoto wetu kwa namna ambayo sisi tungependa kutendewa katika mazingira husika, Mathayo 7:12.

Unyanyasaji wa watoto kihisia

Hivi unajua kuwa tangu utoaji mimba ulipohalalishwa ukatili wa watoto umeongezeka kwa asilimia 300. Hivi si wazazi wasiokuwa na tatizo kuua mtoto mmoja watadhani kuwa ni jambo dogo kumfanyia ukatili mwingine?

Zipo sababu nyingi zinazoweza kumsababisha mzazi kumnyanyasa mtoto kihisia. Labda ni “tabia ya kujifunza.” Pengine hivyo ndivyo wazazi walivyowalea watoto wao na walivyochagua kuwalea watoto wao? Mara nyingi, unyanyasaji wa kihisia hutokea kwenye ndoa zilizovunjika ambapo mzazi wa kambo anakuwepo na anakuwa hana muda wa kuelewa utii wa kifamilia na hivyo kuwabugudhi watoto. Wakati fulani mzazi anayeishi peke yake huwatwika fadhaa, kisirani na maumivu watoto wao. Kisha kunakuwa na ushawishi wa madawa ya kulevya na pombe.

Uhalisia ni kwamba kuna watoto wengi wanaonyanyaswa na wazazi wao kila uchao. Na huu siyo unyanyasaji unaotokana na umasikini. Unyanyasaji wa jinsi hii huweza kutokea kwenye matofali ya udongo, nyumba za matembe Africa, au katika majumba ya mamilioni ya dola Marekani. Watoto wengine wanaamka kwa hofu ya kujua kuwa sasa kumekucha kusikia mijitusi kutoka kwa wazazi wao “Wewe si lolote wala chochote,” “ mbumbumbu,” Hata huvutii,” “Mshenzi,” n.k. Na hawa watoto wanakua huku wakiwa na hizi hisia hasi zikiwa ndiyo taswira ya mitazamo yao. Hivyo wanateseka kwa kuwa na mioyo iliyovunjika, kudharauliwa, kukandamizwa, mawazo ya kutaka kujiua na mengineyo.

Wazazi wenzangu, sisi ni wajenzi wa hatima ya watoto wetu. Na kila anayedai kupenda kwa upendo wa Bwana, hatazikwaza nafsi zisizo hatia na roho safi za vijana, na kuwafanya baadaye wawe watu wenye kisirani, wenye chuki, au waliochanganyikiwa na wenye wasiwasi. Badala yake, kama mishale mkononi mwa shujaa (Zaburi 127:3-5) tutafanya kila tuwezalo kuwaelekeza kwa Mungu!

Katika Warumi 13:10, Paulo alisema “Pendo halimfanyii jirani neno baya.” Hivi hili halihusiani na uhusiano wetu na watoto? Tena, katika 2 Wakorintho 10:5 tunatakiwa “kuteka nyara kila fikra ipate kumtii Kristo,” Hivi, hilo halihusiani na watoto wetu?. Hebu, tukumbuke Wakolosai 3:21 “Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije wakakata tama.” Au kwa lugha rahisi ingesemwa “ msiwajaze visirani watoto wenu wasije wakakata tama. Wakati wote wazazi, tukumbuke ya kwamba ni Bwana aliyewaumba watoto wetu, na aliwafanya tangu wakiwa tumboni na ndiye atakayekuwa msaada wao, Isaya (44:2). Na tumsaidie Mungu ili awasaidie kuwa bora kama inavyowezekana, na nidhamu ni muhimu na inahitajika. Lakini kuwajaza visirani huwaharibu na unaweza ukawa ndiyo msingi unaowapeleka upotevuni. Tuwaelekeze kwa Mungu!

Unyanyasaji wa mtoto-Ngono

Nilipokuwa naanza kaundika kuhusiana na unyanyasaji wa watoto nilijua kuwa kuna unyanyasaji wa aina nne niliotaka kuuzungumzia; unyanyasaji wa kimwili,

hisia, kiroho na ngono. Lakini unyanyasaji wa kingono ni jambo tusilotaka kulizungumzia leo. Hata hatutaki kufiria uwepo, uhalisia na tishio la unyanyasaji wa jinsi hii. Tunatakiwa kuuzungumzia kwa ajili ya usalama wa watoto wetu, na kwa sababu ya tishio kubwa la unyanyasaji huu lililopo leo.

Ifuatayo ni takwimu kutoka kwenye tovuti ya CDC. 20% ya unyanyasaji wa watoto kingono. Kila mwaka kunakuwa na taarifa milioni tatu kuhusiana na unayanyasaji wa watoto. Katika nchi za ulimwengu wa kwanza, Marekani ni moja ya nchi zinazoongoza kwa kuwa na rekodi mbaya kabisa ya unyanyasaji wa watoto. Kila baada ya sekunde kumi, mtoto mmoja anafanyiwa unyanyasaji wa kingono Marekani. 80% ya watu wenye umri wa miaka 21, wamewahi kufanyiwa unyanyasaji wa kingono na wana matatizo ya kisaikolojia. Watoto waliofanyiwa unyanyasaji wa kingono huwa wahalifu mara 9.

Tunatakiwa kuwalinda watoto wetu dhidi ya mafataki. Wanaweza kuwa mafataki wa kiume wa kike. Unaweza ukawa ulawiti au ushoga. Lakini kutokana na kuzuka kwa picha za ngono na kumomonyoka kwa maadili, karibia kila jamii ina wanyanyasaji wa watoto kingono wakiishi miongoni mwao. Kwa kujua hili ni kweli, hatutakiwi kuwa wendawazimu kwa kumshuku kila mtu, lakini hatuwezi kuishi huku tumefumba macho yetu na kujidanganya kwamba janga hili halitawapata wa kwetu.

Leo kila mzazi awe na mazungumzo fulani yale ambayo hataki kuongelea na watoto wake. Lakini tunatakiwa kuzungumza na watoto wetu na kuwajulisha linaloweza kuwatokea. Wahadharishe juu hali fulani fulani, wakatae minenguo inayohamasisha ngono na kutoa taarifa ya jambo hilo haraka iwezekanavyo.

Kila andiko linalokataza uasherati linakataza unyanyasaji wa watoto kingono, Warumi 13:9. Nasi kama wazazi tumeamriwa siyo tu kulinda mioyo yetu, bali na ile ya watoto wetu.

Unanyanyasaji wa watoto- Kiroho;

Tumepewa watoto tuwapende, sio tuwanyanyase. Watoto ni mbegu, na Mungu anatafuta leo mbegu yenye utauwa, Malaki 2:15. Watoto wanafananishwa na mishale mikononi mwetu na tunatakiwa tuwaelekeze kwa Mungu, Zaburi 127:1-5. Kama wazazi, tunatakiwa kuwalea watoto wetu katika maonyo ya Bwana, Waefeso 6:4. Na kama tukishindwa kuwapa mahitaji watoto wetu ikiwa ni pamoja na ya kiroho, basi tunahukumiwa na Mungu kama wabaya kuliko mtu asiye amini, 1 Timotheo 5:8.

Ingawaje unyanyasaji wa kingono, kimwili na kihisia ni jinai, Unyanyasaji wa kiroho ndiyo unyanyasaji pekee ambao umehalalishwa hapa nchini kwetu. Hauvunji sheria yoyote ya kibinadamu. Na bado, kama ilivyo kwa aina zingine za unyanyasaji kwa watoto, Mungu hatauachilia unyanyasaji wa watoto kiroho kama Taifa letu linavyoachilia.

Kuna watoto makundi kwa makundi ambao wametelekezwa kiroho. Hawapewi chakula cha mbinguni, Mathayo 4:4. Wengine wamefundishwa matapishi ya shetani, nayo yanawaharibu vile vile, Yohana 8:32. Wapo ambao huwaacha watoto wao wakaenenda katika njia za dhambi na wanashindwa kuwadhibiti watoto, 1 Samuel 3:13. Wengine huwaacha watoto wao wanajitosa katika ubadhilifu wa ulimwengu. Kwa kuwaacha watoto wakawa na uhuru wa filamu,marafiki, chaneli za luninga, muziki au michezo wanavyotaka. Ingawaje maandiko yanatuonya "Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; maana ndiko zitokako chemchemi za uzima". Watoto wako hivyo. Na kwa sababu ya umri na kutokukomaa kwao wanatuhitaji kulinda akili zao kabisa.

Kila mzazi aliye mkristo lazima ajitahidi kuonyesha ushawishi wa Kikristo kwa watoto wake. Kwa maana hakuna yeyote kati yetu anayetaka kusimama mbele za Mungu akiwa ametelekeza kiroho watoto wake na kuwakwaza.